

**SALAMU ZA BI. SUZANNE NDOMBA DORAN, MTENDAJI MKUU WA
CHAMA CHA WAAJIRI TANZANIA (ATE) KATIKA KILELE CHA
MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI
DUNIANI, 2024- ARUSHA.**

1. **Mhe. Doto Biteko. Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati**
2. **Mhe.Jenista Mhagama. Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu.**
3. **Mhe. Patrobas Katambi Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Vijana Ajira na Wenye Ulemavu.**
4. **Mhe. Paul Christian Makonda Mkuu wa Mkoa Arusha**
5. **Mhe. Thomas Ole Sabaya Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha.**
6. **Bi Edith Simtenga. Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana,Ajira na Wenye Ulemavu.**
7. **Dkt Adlehem Meru.Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri OSHA.**
8. **Bi Caroline Khamati Mugalla. Mkurugenzi wa shirika la kazi Duniani.**
9. **Bi. Juliana Mpanduji. Mwakilishi wa rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA),**
10. **Wakuu wa Taasisi za Serikali na Binafsi, Ndugu Waajiri na Wafanyakazi,**
11. **Ndugu Waandishi wa Habari, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana**

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kujumuika hapa Jijini Arusha katika Viwanja hivi vya General Tires siku hii ya leo ambapo Nchi yetu inaungana na Dunia kuadhimisha Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi

(OSHA) kwa kutambua na kutushirikisha Wadau muhimu tukiwemo sisi wa Chama Cha Waajiri Tanzania (ATE) na Shirikisho la Vyama vyatya Wafanyakazi (TUCTA) pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO), kwa hakika maonesho haya yamefana sana, Hongereni sana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi.

Maadhimisho ya mwaka huu yamebeba kauli mbiu inayosema: “*Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi katika Usalama na Afya Kazini: Sajili eneo la Kazi OSHA katika harakati za kupunguza athari hizo*”

Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kinatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Rasilimali watu katika kukuza Uchumi na kuleta maendeleo. Na kwa kutambua hilo tumeendelea kutoa elimu juu ya Usalama na Afya Mahala pa kazi na kanuni zake kwa Waajiri na kwa Kushirikiana na Wakala wa Usalama wa Afya mahala pa kazi, tumefanya mafunzo na vikao ili kutataua changamoto za waajiri na wafanyakazi mahala pa kazi zinazohusu Usalama na Afya.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mabadiliko ya tabia nchi yana athari kubwa kwenye usalama wa kazini. Hapa nitaeleza kwa ufupi baadhi ya athari hizo:

Mosi, ni Mabadiliko ya Hali ya Hewa: ambapo Mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa yanaweza kuleta hatari kazini. Mafuriko, dhoruba kubwa, au mvua nyingi, zinaweza kuathiri usalama wa wafanyakazi na miundombinu ya kazi, na kuathiri uzalishaji katika sekta ya Uchumi. Na hili tunalishuhudia na mvua nyingi zinaendelea kunyesha kwa kiwango cha juu.

Pili, ni Ongezeko la Joto: Kuongezeka kwa joto kunaweza kusababisha mazingira ya kazi kuwa na joto hususani wafanyakazi wa viwandani au wanaofanya kazi nje, wavuvi na Wafanyakazi wengi walio katika sekta isiyo rasmi. Joto jingi linaweza kuleta uchovu na

kusathiri afya za watu na kusababisha madhara kiafya na hatimaye kueta m dororo wa kazi na kuathiri tija.

Tatu, Uchafuzi wa hewa; Mabadiliko ya Tabia nchi yanaweza kusababisha uchafuzi wa hewa na kuathiri afya za watu na kuleta kemikali hatarishi zinaweza kusababisha matatizo ya kupumua au magonjwa mengine .

Na pia, Athari za mabadiliko ya tabia nchi zinaweza kuathiri mazingira na kusababisha kuongezeka kwa magonjwa kama vile malaria au dengue, mafua. Hii inaathiri afya na kusababisha madhara sio tu kwa mfanyakazi bali pia katika biashara kutokana na kupoteza nguvu kazi na kuathiri uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, ya mwaka 2003 inamtaka mwajiri kuweka mazingira salama na yenye afya kwa wafanyakazi na pia inamtaka Mfanyakazi kulinda afya yake na ya mwenzake mahala pa kazi kwa kufuata kanuni na maagizo yanayotolewa na Mwajiri katika kulinda Usalama kwa kutumia vifaa kinga mahala pa kazi.

Chama Cha Waajiri (ATE) kinatambua umuhimu wa kutekeleza sheria, kuhamasisha Waajiri kuzingatia sheria na kuhakikisha Usalama na Afya unakuwepo mahali pa kazi ili kulinda uzalishaji, kuwepo kwa amani na utulivu sehemu ya kazi, na kuongeza ustawi wa Wafanyakazi na Afya zao ili kuepeuka migogoro isiyo ya lazima.

Nitumie fursa hii kutoa rai kwa Waajiri kuweka mikakati ya kukabiliana na dharura, ikiwemo mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la joto.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Napenda kuhitimisha salamu za ATE, kwa kuwapongeza OSHA na Wadau wote wa UTATU kushiriki maadhimisho haya. Pia niwapongeze wote watakaoshinda tuzo lakini pia wote walioshiriki.. nyote ni washindi.

Asanteni kwa kunisikiliza